

Maana ya huduma unganishi na rufaa.

Huduma unganishi na rufaa ni huduma inayojumuisha ushauri, matibabu na huduma za Msaada zinazotolewa katika ngazi mbalimbali kuanzia kwenye vituo vya huduma za afya Hadi kwenye jamii.

Huduma hizi hutolewa na WAHUUWANYU na watoa huduma katika vituo vya afya.

Huduma unganishi na rufaa itakuwezesha;

- Kuboresha na kuimarisha afya yako kwa kupata huduma za ziada.
- Kuunganishwa na huduma za msingi mfano matibabu, huduma za kisaikolojia, kisheria,, kiroho na ushauri wa lishe,

- Kuboresha na kukuimarisha kiuchumi
- kwa kukuunganisha na vikundi vya ujasiriamali.
- Kupunguza unyanyapaa na ubaguzi
- Kuzingatia ratiba ya kuhudhuria kiliniki na ufuasi sahihi wa dawa.
- Kuongeza uelewa wa kinga na matibabu na huduma endelevu.

Aina za huduma unganishi na rufaa

